© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

Usool ya kwanza

Basi ukiulizwa nani Mola wako?

Jibu kwa kusema: Mola wangu ni Allaah, aliyenileya mimi na viumbe vyote kwa neema na fadhila zake. Na yeye pekee ninaye muabudu na hakuna mwengine ninaye muabudu pembeni mwake. Na dalili ni kauli ya Allaah (ta'ala)

ٱلْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ ٱلْعَٰلَمِينَ ﴿٢﴾

Sifa njema zote ni za Allaah, Mola wa viumbe vyote. (Surah Fatiha 1:2) na kila kitu pembeni ya Allaah kime umbwa na mimi ni mmoja katika maumbile.

Na basi ukiulizwa: vipi ulimjuwa Mola wako Mlezi (yaani Allaah)?

Jibu kwa kusema: kutokamana na ishara (alama) zake na kwa vitu alivyoviumba; na kwenye ishara (alama) zake ni usiku na mchana na pia jua na mwezi, na katika vitu Alivyoviumba ni mbingu saba na ardhi saba na kila kilichomo ndani, na baina ya mbingu na ardhi . Na dalili ni kauli ya Allaah

وَمِنْ ءَايَٰتِهِ ٱلَّيْلُ وَٱلنَّهَارُ وَٱلشَّمْسُ وَٱلْقَمَرُ ۚ لَا تَسْجُدُوا۟ لِلشَّمْسِ وَلَا
لِلْقَمَرِ وَٱسْجُدُوا۟ لِلَّهِ ٱلَّذِى خَلَقَهُنَّ إِن كُنتُمْ إِيَّاهُ تَعْبُدُونَ ﴿٣٧﴾

Na katika Ishara zake ni usiku na mchana, na jua na mwezi. Basi msilisujudie jua wala mwezi, bali msujudieni Allaah aliye viumba, ikiwa nyinyi mnamuabudu Yeye tu. (Surah Fussilat 41:37)

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

Na kauli ya Allaah (ta'ala)

إِنَّ رَبَّكُمُ ٱللَّهُ ٱلَّذِى خَلَقَ ٱلسَّمَٰوَٰتِ وَٱلْأَرْضَ فِى سِتَّةِ أَيَّامٍ ثُمَّ ٱسْتَوَىٰ عَلَى
ٱلْعَرْشِ يُغْشِى ٱلَّيْلَ ٱلنَّهَارَ يَطْلُبُهُۥ حَثِيثًا وَٱلشَّمْسَ وَٱلْقَمَرَ وَٱلنُّجُومَ
مُسَخَّرَٰتٍۭ بِأَمْرِهِۦٓ ۗ أَلَا لَهُ ٱلْخَلْقُ وَٱلْأَمْرُ ۗ تَبَارَكَ ٱللَّهُ رَبُّ ٱلْعَٰلَمِينَ ﴿٥٤﴾

Hakika Mola wenu ni Allaah aliye ziumba mbingu na ardhi katika siku sita. Kisha akapaa juu ya arshi (Kiti cha Enzi) [kwa njia inayolingana na Utukufu wake (1) Huufunika usiku kwa mchana, ufuatao upesi upesi. Na jua, na mwezi, na nyota zinazo tumika kwa amri yake. Fahamuni! maumbile na amri ni zake. Ametukuka kabisa Allaah, Mola wa viumbe vyote. (Surah al-A'raaf 7:54)

Na Mola Mlezi (yaani Allaah) ni yule ambaye ana abudiwa, na dalili ni kauli ya Allaah (ta'ala)

يَٰٓأَيُّهَا ٱلنَّاسُ ٱعْبُدُوا۟ رَبَّكُمُ ٱلَّذِى خَلَقَكُمْ وَٱلَّذِينَ مِن
قَبْلِكُمْ لَعَلَّكُمْ تَتَّقُونَ ﴿٢١﴾ ٱلَّذِى جَعَلَ لَكُمُ
ٱلْأَرْضَ فِرَٰشًا وَٱلسَّمَآءَ بِنَآءً وَأَنزَلَ مِنَ ٱلسَّمَآءِ مَآءً
فَأَخْرَجَ بِهِۦ مِنَ ٱلثَّمَرَٰتِ رِزْقًا لَّكُمْ ۖ فَلَا تَجْعَلُوا۟
لِلَّهِ أَندَادًا وَأَنتُمْ تَعْلَمُونَ ﴿٢٢﴾

Enyi watu! Muabuduni Mola wenu Mlezi aliye kuumbeni nyinyi na wale wa kabla yenu, ili mpate kuokoka (kuwa na taqwa). Na ni Yeye ambaye amekufanyieni hii ardhi kuwa kama tandiko, na mbingu kama paa, na akateremsha maji kutoka mbinguni, na kwa hayo akatoa matunda yawe riziki zenu. <u>Basi msimfanyizie Allaah washirika, na hali nyinyi mnajua</u> (kuwa hana mshirika). (Surah al-Baqara 2: 21-22)

Alisema Ibn Katheer rehma ya Allaah iwe juu yake; Mwumbaji wa hivi vyote ni yeye peke anayestahiki kuabudiwa (yaani Allaah) "Na aina zote za Ibadah tofauti alizo amrisha Allaah kama Al Islam na Al Iman na Ihsan, na zingine

kwa mfano :- **kuomba dua -** (Dua), **khofu -** (khawf), **kutarajia -** (rajaa). **Kutegemeya -** (tawakul), **shauku -** (raghbah), **kikuli -** (rahbah), **kunyeyekea** - (khusoo), **uchaji -** (khashyah), **uregevu wa kutubia -** (inaabah), **kuomba msaada -** (isti'aanah), **kuomba kinga -** (isti' aadhah), **koumba msaada na maokozi -** (istighaathah), **dhabihu -** (dhabh) **kuweka nadhiri – (**nadhr) na Ibadah zenginezo alizo amrisha Allaah, zote zitendwe kwa kuelekezwa kwake Allaah (ta'ala).

Na yeyote anaye elekeza Ibadah yake kwa mwingine asiye Allaah (ta'ala) basi yeye amekuwa **Mshrikina**, na **Kafiri** na dalili ni kauli ya Allaah (ta'ala)

وَمَن يَدْعُ مَعَ ٱللَّهِ إِلَٰهًا ءَاخَرَ لَا بُرْهَٰنَ لَهُۥ بِهِۦ فَإِنَّمَا حِسَابُهُۥ عِندَ
رَبِّهِۦٓ ۚ إِنَّهُۥ لَا يُفْلِحُ ٱلْكَٰفِرُونَ ﴿١١٧﴾

Na anaye muomba - pamoja na Allaah - mungu mwenginewe hana ushahidi wa hili; basi bila ya shaka hisabu yake iko kwa Mola wake. Kwa hakika makafiri hawafanikiwi. (Surah al-Muminoon 23:117)

Na kwenye Hadithi inayosema"**Dua ni kiini ya Ibadah. (2)**" Na dalili ni kauli ya Allaah (ta'ala)

وَقَالَ رَبُّكُمُ ٱدْعُونِىٓ أَسْتَجِبْ لَكُمْ ۚ إِنَّ ٱلَّذِينَ يَسْتَكْبِرُونَ عَنْ عِبَادَتِى
سَيَدْخُلُونَ جَهَنَّمَ دَاخِرِينَ ﴿٦٠﴾

Na Mola wenu anasema: Niombeni nitakuitikieni. Kwa hakika wale wajivunao na kuniabudu Mimi wataingia Jahannamu wadhalilike (Surah Ghaafir 40:60)

Dalili ya khofu (khawf) ni kauli ya Allaah (Ta'ala)

فَلَا تَخَافُوهُمْ وَخَافُونِ إِن كُنتُم مُّؤْمِنِينَ ﴿١٧٥﴾

basi msiwaogope, bali niogopeni Mimi mkiwa nyinyi ni Waumini. (Surah al-Imran 3:175)

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

Dalili ya kutarajia (rajaa) ni kauli ya Allaah (ta'ala)

فَمَن كَانَ يَرْجُوا۟ لِقَآءَ رَبِّهِۦ فَلْيَعْمَلْ عَمَلًا صَٰلِحًا وَلَا يُشْرِكْ
بِعِبَادَةِ رَبِّهِۦٓ أَحَدًۢا ﴿١١٠﴾

Mwenye kutaraji kukutana na Mola wake basi naatende vitendo vyema, wala asimshirikishe yeyote katika ibadah ya Mola wake. (Surah al-Kahf 18:110)

Dalili ya kutegemeya (tawakul) ni kauli ya Allaah (ta'ala)

وَعَلَى ٱللَّهِ فَتَوَكَّلُوٓا۟ إِن كُنتُم مُّؤْمِنِينَ ﴿٢٣﴾

Na mtegemeeni Allaah ikiwa nyinyi ni Waumini. (Surah al-Maidah 5:23)

Na kauli ya Allaah (ta'la)

وَمَن يَتَوَكَّلْ عَلَى ٱللَّهِ فَهُوَ حَسْبُهُۥٓ

Na anaye mtegemea Allaah Yeye humtosha. (Surah at-Talaaq 65:3)

Dalili ya shauku (raghbah) , kiku**l**i (rahbah), na kunyeyekea (khusoo) ni kauli ya Allaah (ta'ala)

إِنَّهُمْ كَانُوا۟ يُسَٰرِعُونَ فِى ٱلْخَيْرَٰتِ وَيَدْعُونَنَا رَغَبًا وَرَهَبًا ۖ
وَكَانُوا۟ لَنَا خَٰشِعِينَ ﴿٩٠﴾

Hakika wao walikuwa wepesi wa kutenda mema, na wakituomba kwa shauku na khofu. Nao walikuwa wakitunyenyekea (Surah al-Anbiya 21:90)

Dalili ya uchaji (khashyah) ni kauli ya Allaah (ta'ala)

فَلَا تَخْشَوْهُمْ وَٱخْشَوْنِ

basi msiwaogope, bali niogopeni Mimi (Surah al-Maidah 5:3)

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

Dalili ya uregevu nakutubu (inaabah) ni kauli ya Allaah (ta'ala)

وَأَنِيبُوٓاْ إِلَىٰ رَبِّكُمۡ وَأَسۡلِمُواْ لَهُۥ

Na rejeeni na kutubia kwa Mola wenu, na silimuni kwake (Surah az-Zumar 39:54)

Dalili ya kuomba msaada (isti'aanah) ni kauli ya Allaah (ta'ala)

إِيَّاكَ نَعۡبُدُ وَإِيَّاكَ نَسۡتَعِينُ ٥

Wewe tu tunakuabudu, na Wewe tu tunakuomba msaada (Surah al-Fatiha 1:5)

Na kwenya hadithi inayosema "**na ukiomba msaada basi omba msaada kutoka kwa Allaah"** [imepokelewa na timidhi and kusahihishwa na Shaykh al-Albanee kwenye al-Mishkaat (no.5302)]

Dalili ya koumba kinga (isti'aadhah) ni kauli ya Allaah (ta'ala)

قُلۡ أَعُوذُ بِرَبِّ ٱلۡفَلَقِ ١

Sema: Najikinga kwa Mola wa mapambazuko (Surah al-Falaq 113:1)

Na

قُلۡ أَعُوذُ بِرَبِّ ٱلنَّاسِ ١

Sema: Ninajikinga kwa Mola wa wanaadamu (Surah an-Naas 114:1)

Dalili ya kuomba uokozi (istighaathah) ni kauli ya Allaah (ta'la)**.**

إِذۡ تَسۡتَغِيثُونَ رَبَّكُمۡ فَٱسۡتَجَابَ لَكُمۡ

Mlipo kuwa mkimuomba maokozi Mola wenu , naye akakujibuni . (Surah al-Anfal 8:9)

Dalili ya dhabihu (dhabh) ni kauli ya Allaah (ta'ala)

قُلۡ إِنَّ صَلَاتِي وَنُسُكِي وَمَحۡيَايَ وَمَمَاتِي لِلَّهِ رَبِّ ٱلۡعَٰلَمِينَ ١٦٢

Sema: Hakika Sala yangu, na dhabihu yangu, na uhai wangu, na kufa kwangu, ni kwa ajili ya Allaah, Mola wa viumbe vyote. (Surah al-An'aam 6: 162)

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

Na pia Mtume Sallalahu Alalihi Wasallam alisema : **La'na ya Allaah iko juu ya yule anaye chinja dhabihu kwa mwengine asiyekuwa Allaah** (Imepokelewa na Muslim)

Ushahidi wa nadhiri **(**nadhr) ni kauli ya Allaah (ta'la)

يُوفُونَ بِٱلنَّذۡرِ وَيَخَافُونَ يَوۡمٗا كَانَ شَرُّهُۥ مُسۡتَطِيرٗا ۝٧

Wanatimiza nadhiri, na wanaiogopa siku ambayo shari yake inaenea sana (Surah al-Insan 76 :7)

Kumbukumbu

(1) Kauli Ya Imam Maalik -- Imaam darul Hijrah (Madinah)

Al-istiwa ni maarufu, na vipi ilitendeka haiwezi kufahamika, kuitaqidi (kama iletendeka) ni waajib, na kuuliza (ilitendeka vipi) ni Bidaa (uzushi)

Alistiwa ni maarufu => yaani ni kitu maarufu kwenye lugha – ina maanisha kupaa.

na vipi ilitendeka haiwezi kufahamika => kwa kutumiya akili, na wala haiku shereheshwa ilitendeka vipi katika wahyi (Quran na Sunnah) – basi vipi ilitendeka haijulikani .

kuuliza (ilitendeka vipi) ni Bidaa => haiujulikani (halikuulizwa hili swali) wakati wa Mtume Sallalahu Alalihi Wasallam na maswahaba wake.

Haya maneno (ya Imaam Maalik) kwa ujumla huu ni kanuni (qaida) juu ya sifa zote za Allaah. => Allaah ametuthibitishia (sifa zake) ama kupitia kwa Mtume wake. Allaah ametueleza kwamba ana sifa lakini hakutueleza sifa zake ziko vipi.

Kuzungumzia sifa za Allaah inafwatiwa na kumzungumziya Allaah mwenyewe => Kama vile tuna thibitisha kuwa Allaah yupo bila ya kuuliza yupo vipi, basi tufanya vivyo hivyo pia na sifa zake zenginezo (yaani hatulizi sifa za Allaah ziko vipi).

Sharh Aqida Hamawiyaah ya shaykh ul-Islaam Ibn Taymiyyah

© Manhaj ya Salafi e-Books 2002. www.manhajyasalafi.com

(2) Hii hadithi kwa usemi **Dua ni kiini ya Ibadah** iliyo pokelewa na Tirmidhi ni *dhaifu*. Amesema Shaykh Muhammad Naasirudeen al-Albanee kwenye al-Mishkat (nambari 2331) kwa ajili ya udhaifu wa mmoja wa mpokelevu kwenye Isnad (salasila) yake kwa jina Ibn Lahee'ah.

Imaam Ahmad kwenye as-Sunan yake, amepokea hadeeth **sahihi** kwa usemi: **Dua Ni Ibadaah** [Shaykh al-Albanee amesema ni sahihi kwenye Saheehul Jaami' (nambari 3407)]